JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

# MWONGOZO WA KITAIFA WA UBAINISHAJI NA UPIMAJI WA WATOTO/ WANAFUNZI WENYE MAHITAJI MAALUMU YA KIELIMU

JUNI, 2023

**Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, 2023**

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupiga chapa au kutoa Mwongozo huu kwa namna yoyote ile bila idhini ya Katibu Mkuu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

**ISBN** …………………..

**Toleo la Pili 2023**

Umechapishwa na:

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,

Mji wa Serikali Mtumba,

Mtaa wa Afya,

S.L.P 10,

**40479 DODOMA, TANZANIA.**

# YALIYOMO

**ORODHA YA VIFUPISHO.......................................... vi**

**SHUKRANI........................................................... vii**

**DIBAJI..................................................................xiii**

**SURA YA KWANZA.................................................... 1**

1.0 Utangulizi.......................................................... 1

1.1 Usuli...................................................................1

1.2 Umuhimu wa Mwongozo.................................... 1

1.3 Muundo wa Mwongozo...................................... 2

1.4 Malengo ya Mwongozo.......................................2

1.4.1 Lengo Kuu......................................................... 2

1.4.2 Malengo Mahususi..............................................3

1.5 Watumiaji wa Mwongozo.................................... 3

1.6 Wanufaika wa Mwongozo...................................4

**SURA YA PILI........................................................... 5**

2.0 Utaratibu wa Ubainishaji, Upimaji na Utoaji wa Afua Stahiki.....................................................5

2.1 Viashiria vya Watoto/wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu ya Kielimu.......................................... 5

2.2 Ubainishaji, upimaji, utoaji wa afua stahiki na tathmini........................................................ 12

2.2.1 Hatua ya Kwanza: Ubainishaji........................... 12

2.2.1.1 Taarifa zinazopaswa kukusanywa na kusajiliwa.13
2.2.2 Hatua ya Pili: Upimaji.......................................... 13
2.2.3 Hatua ya Tatu: Utoaji wa Afua stahiki.................. 14
2.2.4 Hatua ya Nne: Ufuatiliaji na Tathmini...................15

**SURA YA NNE.............................................................. 18**
4.0 Majukumu na Wajibu wa Watumiaji wa Mwongozo........................................................ 18
4.1 Ngazi ya Wizara..................................................18
4.1.1 Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (WyEST)........................................................... 18
4.1.2 Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI)........................................19
4.1.3 Ngazi ya Mkoa.................................................... 19
4.1.4 Ngazi ya Halmashauri..........................................20
4.1.5 Ngazi ya Kata..................................................... 21
4.1.6 Ngazi ya Vijiji/Mitaa.............................................22
4.1.7 Ngazi ya Shule.................................................... 22
4.2 Kituo cha Upimaji.............................................. 23

**SURA YA TANO:...........................................................24**
5.0 Ufuatiliaji, Tathmini na Utunzaji wa Kumbukumbu 24
5.1 Ufuatiliaji............................................................. 24
5.2 Tathmini.............................................................. 24
5.3 Malengo ya ufuatiliaji na tathmini ni:....................25

5.4 Utunzaji wa Kumbukumbu.................................25

**REJEA.............................................................. 26**

**VIAMBATISHO................................................... 27**

**Kiambatisho 1:** Fomu A1 Fomu ya Ubainishaji wa Awali..............................................................27

**Kiambatisho 2:** Fomu B1: Fomu ya ubainishaji wa Awali katika ngazi ya shule za Msingi.................. 27

**Kiambatisho 3:** Fomu C1: Fomu ya upimaji wa mtoto/ mwanafunzi katika Kituo cha Upimaji na Ubainishaji wa Mahitaji Maalumu ya Kielimu kwa Watoto/ wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu.....................27

# ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| BEST | Basic Education Statistics in Tanzania |
| OR-TAMISEMI | Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| UWAWA | Umoja wa Walimu na Wazazi |
| WyEST | Wizara ya Eilimu, Sayansi na Teknolojia |

## SHUKRANI

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inatoa shukrani za dhati kwa wadau wote walioshiriki katika uandaaji wa mwongozo huu. Kipekee, Wizara inatoa shukrani kwa Wakuu wa Shule za Msingi na Sekondari za Serikali na za wamiliki binafsi, Wakufunzi, Wathibiti Ubora wa Shule na Maafisa Elimu kwa ushauri wao uliosaidia kufanikisha uandaaji wa mwongozo huu. Ni matumaini yangu kuwa, shauku kubwa na moyo wa kujituma ulioonekana wakati wa mchakato wa uandaaji wa mwongozo huu utadhihirika wakati wote wa utekelezaji ili kupata matokeo chanya, katika kuhakikisha kila mtoto wa kitanzania anapata elimu bora, kwa kuzingatia usawa.

Mwisho, shukurani za dhati zinatolewa kwa Mfuko wa Serikali ya Watu wa Uingereza (Ukaid) kupitia Msaada wa kitaalamu kutoka Program ya Shule Bora ambao kwa kiasi kikubwa umefanikisha uandishi wa mwongozo huu.

.........................................

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa

**KAMISHNA WA ELIMU**

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

# DIBAJI

Katika haki ya elimu kwa wote, na mwamko wa elimu jumuishi, Tanzania imefanya juhudi kubwa za sera, sheria na programu kuelekea kuboresha utoaji wa huduma za kielimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu ya kielimu katika ngazi zote za elimu. Kufuatia kurekebisha, kuunda upya na kupitisha Mkakati wa Kitaifa wa Elimu Jumuishi (MKEJ): 2021/22-2025/26; kupitia Kitengo chake cha Elimu Maalumu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, sasa imepitia na kurekebisha 'Miongozo ya Msaada wa Elimu, Utambuzi na Ubainishaji' wa 2013. Matokeo yake, 'Mwongozo wa Utambuzi na Ubainishaji wa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu ya Kielimu,' 2023 unatarajiwa kusaidia kwa ubora zaidi na kwa ufanisi kazi muhimu zinazohusiana na utambuzi na ubainishaji wa wanafunzi wenye mahitaji maalumu ya kielimu. Mwongozo huu utasaidia wadau wote muhimu, hasa wazazi/walezi, vituo vya elimu katika ngazi zote, Vituo vya ubainishaji na upimaji ili kubaini mahitaji maalumu ya kielimu na watendaji wengine wote ikiwemo Mashirika yasiyo ya kiserikali katika kufanya ubainishaji kwa wakati na kwa usahihi zaidi.

Uboreshaji wa Mwongozo huu unatambuliwa kwa

kile tulichojifunza kwa muda wa miaka tisa ya kutumia Miongozo ya Msaada wa kielimu, Utambuzi na Ubainishaji, pamoja na mazoezi ya kitaifa katika ubainishaji wa mahitaji maalumu ya kielimu kwa watoto/wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Zaidi ya hayo, mashauri na majadiliano ya kina na wataalamu na watendaji husika yalifanywa ili kuongeza uzoefu wao, maarifa, ufahamu na ujuzi juu ya masuala maalumu ya kielimu.

Mwongozo huu umetengenezwa kwa kufuata hatua mbili za viwango, hatua ya kwanza inahusisha ubainishaji wa msingi, utambuzi nyumbani na jamii husika. Hatua hii itatekelezwa zaidi na watu wenye mafunzo ya msingi ili kuhakikisha tuna uwezo wa haraka, lakini kwa usahihi, kupanua wigo na kuuelekeza ngazi ya chini kabisa katika mchakato wa utambuzi na ubainishaji wa watoto/wanafunzi wenye mahitaji maalumu ya kielimu. Hatua ya pili ni Ubainishaji maalumu ambao hufanywa na timu ya wataalamu, ikiwa ni pamoja na walimu na wataalamu wa afya/utabibu. Kwa ujumla, Mwongozo huu umeundwa kuwa rasilimali ya msingi ili kusaidia wadau husika kupata uelewa wa kutambua na kubainisha watoto/wanafunzi wenye mahitaji maalumu ya kielimu kuelekea utoaji wa afua stahiki.

Nawasihi wadau wote wa elimu kuutumia Mwongozo huu. Aidha, utekelezaji wa dhati wa Mwongozo huu utapelekea utoaji wa elimu kwa wote bila ubaguzi, na utachangia kwa kiasi kikubwa katika ujenzi wa taifa letu la Tanzania ambayo ni ya haki, usawa na ujumuishi.

..............................................

Prof. Carolyne I. Nombo

**KATIBU MKUU**

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

# SURA YA KWANZA

## 1.0 Utangulizi

Sura hii inafafanua usuli, umuhimu na muundo wa mwongozo. Vilevile, Sura hii imeainisha malengo ya mwongozo, watumiaji na wanufaika wa mwongozo katika muktadha wa utoaji wa huduma kwa watoto/wanafunzi wenye mahitaji maalumu ya kielimu.

## 1.1 Usuli

Mwongozo wa kitaifa wa ubainishaji na upimaji wa watoto/wanafunzi wenye mahitaji maalumu ya kielimu wa mwaka 2023 unalenga kutoa dira juu ya ubainishaji na upimaji na jinsi ya kutoa afua stahiki kwa watoto/wanafunzi wenye mahitaji maalumu ya kielimu. Aidha, mwongozo unaainisha malengo, namna ya kufanya ubainishaji na upimaji wa watoto/wanafunzi wenye mahitaji maalumu ndani na nje ya shule/vyuo kwa lengo la kutoa afua stahiki. Pia mwongozo huu unafafanua majukumu ya wadau mbalimbali na namna ya kufanya ufuatiliaji na tathmini.

## 1.2 Umuhimu wa Mwongozo

Mwongozo huu ni sehemu ya utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Elimu Jumuishi (MKEJ) 2021/2022 - 2025/26 ambao umetanua wigo wa ngazi za elimu na makundi ya watoto/wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika utoaji wa afua stahiki. Aidha, mwongozo huu ni nyenzo muhimu itakayotumika kuelekeza namna ya kubainisha na kupima watoto/wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika ngazi zote za elimu na jamii ili kutoa afua stahiki. Hivyo,

mwongozo huu ni muhimu kwani utaimarisha utoaji wa elimu katika mazingira maalumu na jumuishi kwa lengo la kuondoa vikwazo vya kimfumo na kimuundo ili kurahisisha ufundishaji na ujifunzaji.

## 1.3 Muundo wa Mwongozo

Mwongozo huu umegawanyika katika sura tano. Sura ya kwanza inafafanua usuli, malengo ya mwongozo, umuhimu wa mwongozo, watumiaji na wanufaika wa mwongozo. Sura ya pili inaeleza utaratibu wa ubainishaji, upimaji na utoaji wa afua stahiki, viashiria vya kubaini watoto/wanafunzi wenye mahitaji maalumu ya kielimu na hatua za utekelezaji wa mwongozo. Sura ya tatu inaelezea muundo wa timu za ubainishaji na mchakato wa ubainishaji na upimaji. Sura ya nne inabainisha majukumu na wajibu wa watumiaji wa mwongozo na Sura ya tano inafafanua namna ya kufanya ufuatiliaji, tathmini na utunzaji wa kumbukumbu.

## 1.4 Malengo ya Mwongozo

Kipengele hiki kinafafanua lengo kuu la mwongozo, malengo mahususi, watumiaji na wanufaika wa mwongozo.

### 1.4.1 Lengo Kuu

Kuimarisha mfumo wa ubainishaji na upimaji kwa watoto/wanafunzi wenye mahitaji maalumu ya kielimu ili kutoa fursa sawa kwa wote na afua stahiki ndani na nje ya mfumo wa elimu.

### 1.4.2 Malengo Mahususi

Mwongozo huu unalenga:

i. Kuainisha taratibu za kufuatwa katika kufanya ubainishaji na upimaji kwa watoto/wanafunzi wenye mahitaji maalumu nchini;
ii. Kubainisha zana zitakazotumika katika kufanya ubainishaji na upimaji wa watoto/wanafunzi wenye mahitaji maalumu;
iii. Kuainisha majukumu ya wadau mbalimbali katika ubainishaji na upimaji kwa watoto/wanafunzi wenye mahitaji maalumu ya kielimu; na
iv. Kuweka utaratibu wa kufuatwa wakati wa kufanya ufuatiliaji na tathimini ya utekelezaji wa mwongozo.

## 1.5 Watumiaji wa Mwongozo

Watumiaji wa mwongozo huu ni:

i. Maafisa elimu katika ngazi ya Taifa, Mkoa, Halmashauri, Kata na viongozi wa Vijiji/Mitaa;
ii. Maafisa Elimu-Elimu Maalumu (Msingi na Sekondari);
iii. Wathibiti ubora wa shule;
iv. Wazazi/Walezi;
v. Mashirika ya Watu wenye Ulemavu;
vi. Wadau wa maendeleo katika elimu, elimu maalumu na jumuishi;
vii. Walimu, wakufunzi, wawezeshaji, wahadhiri, watafiti na watumishi mwega;
viii. Asasi za kiraia na kidini; na
ix. Wabainishaji, wapimaji na waratibu wa vituo vya upimaji.

## 1.6 Wanufaika wa Mwongozo

Utekelezaji wa mwongozo huu unalenga kuwanufaisha watoto/wanafunzi wenye mahitaji maalumu wafuatao: -

i. Watoto/wanafunzi wenye ulemavu;
ii. Watoto/wanafunzi wenye changamoto maalumu katika ujifunzaji;
iii. Watoto/wanafunzi kutoka familia za wafugaji au watu wanaoishi kwa kuhamahama;
iv. Watoto walio nje ya shule;
v. Watoto/wanafunzi wakimbizi;
vi. Watoto/wanafunzi wanaofanya kazi;
vii. Watoto/wanafunzi wenye magonjwa ya kudumu;
viii. Watoto/wanafunzi yatima;
ix. Watoto/wanafunzi wanaoishi katika umasikini uliokithiri;
x. Watoto/wanafunzi wanaoishi mbali na shule;
xi. Watoto/wanafunzi wanaokinzana na sheria;
xii. Watoto wa kike/kiume; na
xiii. Watoto/wanafunzi wenye vipawa na vipaji.

# SURA YA PILI

## 2.0 Utaratibu wa Ubainishaji, Upimaji na Utoaji wa Afua Stahiki

Sura hii inatoa mwongozo kuhusu viashiria vya watoto/wanafunzi wenye mahitaji maalumu ya kielimu, utaratibu wa ubainishaji, upimaji na utoaji wa afua stahiki.

## 2.1 Viashiria vya Watoto/wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu ya Kielimu.

Wabainishaji wanaohusika na kubaini watoto/wanafunzi wenye mahitaji maalumu ya kielimu wanapaswa kufahamu viashiria vya mahitaji maalumu ya watoto/wanafunzi.

Viashiria viainishwe na kujadiliwa kwa kuzingatia mahitaji maalumu ya kielimu wakati wa mafunzo, mikutano ya hadhara ya kijiji/mtaa na kampeni ili kuongeza uelewa kwa wazazi, jamii na watoa taarifa wengine.

**Jedwali Na. 1** linaonesha viashiria vya watoto/wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

| Kundi la Mahitaji Maalumu ya kielimu | Viashiria | Mahali pa kuwapata | Watoa taarifa | Mbinu za kuwabaini |
|---|---|---|---|---|
| **Watoto/ wanafunzi kutoka familia za wafugaji na watu wanaoishi kwa kuhamahama** | Watoto/wanafunzi kutoka kaya za wafugaji na familia zinazohama mara kwa mara/kwa msimu | Nyumbani/ ngazi ya kaya, malishoni; mitaani na kwenye masoko | Viongozi wa jamii; majirani; kundi rika; walimu na watoa huduma wengine katika jamii | Kutembelea mahali anapoishi mtoto/ mwanafunzi; uchunguzi; mahojiano; ripoti/taarifa rasmi na jamii. |
| **Watoto walio nje ya mfumo rasmi wa elimu** | Mtoto mwenye umri wa kwenda shule ambaye hayupo shuleni | Katika kaya, maeneo ya kazi, sokoni, vituo vya usafiri, nk | Wazazi/walezi, watoa huduma za jamii; afisa Maendeleo/Ustawi wa jamii, viongozi wa jamii; walimu, viongozi wa dini, nk | Kutembelea makazi/ mitaa, ushuhudiaji; uhakiki, rejista za Kata/ Kijiji/Mtaa na Kitongoji, watoa taarifa za jamii, daftari la mahudhurio shuleni, ufuatiliaji wa ajira za watoto, Sensa ya Taifa. |
| **Watoto wakimbizi** | Watoto ambao wamekimbia nchi zao wenyewe, wamevuka mpaka wa kimataifa, na kutafuta hifadhi na usalama katika nchi nyingine na watoto wenye hadhi ya ukimbizi wanaokidhi umri wa kwenda shule. | Kambi za wakimbizi | Mashirika ya watoa huduma kama vile UNHCR, IRC, n.k. Watoa huduma za jamii; viongozi wa jamii na mitaa; ripoti za kitaifa, ripoti za sensa, mkuu wa kambi | Kutembelea kambi za wakimbizi; Mahojiano, Kadi za Uthibitisho wa Usajili wa Mkimbizi (PoR), Daftari la Usajili la Kambi ya Wakimbizi. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Watoto wanaofanya kazi** | Mtu aliye na umri wa chini ya miaka 18 anayejihusisha/kutumiwa kufanya kazi kama ajira.<br>Mtoto anayejishughulisha/ anayetumiwa kufanya shughuli za kujipatia kipato kama vile kuombaomba, kuokota makopo au vyuma chakavu, kupakia na kupakua mizigo sokoni, usafirishaji dawa za kulevya, kuosha magari, ngono, kucheza muziki, kung'arisha viatu, uzururaji, kutembeza bidhaa kama machinga na kuiba. | Maeneo ya kazi za mgodini, mwaloni, mashamba makubwa, stendi, masoko, madanguro, maeneo ya starehe, nyumbani/ kwenye kaya, mitaani, nk | Kamati inayohusika na Watoto Wanaoishi katika mazingira hatarishi zaidi; Afisa Ustawi wa Jamii; wazazi; walezi; majirani; makundirika; walimu; watoa huduma za jamii; Afisa Maendeleo ya Jamii; Asasi za Kijamii; Asasi za Kidini; viongozi wa dini; viongozi wa jamii, vijiji na mitaa; maafisa wa magereza. | Kutembelea mitaa, na maeneo mengine ya kazi za kutumikishwa; uchunguzi/ ukaguzi/ ripoti; daftari la mahudhurio darasani. |
| **Watoto/ wanafunzi wenye magonjwa ya kudumu** | Mtoto mwenye historia ya ugonjwa wa muda mrefu ambao umethibitishwa na wataalamu wa afya | Nyumbani; katika kaya; katika kituo cha afya anakoishi mtoto, shuleni | Walezi; majirani; kundirika; walimu; kamati inayohusika na watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi; wahudumu wa vituo vya afya | Kutembelea makazi ya mtoto; kufanya uchunguzi; mahojiano; kuripoti yeye mwenyewe au rufaa; mtoa taarifa wa jamii, ripoti za shule na daftari la mahudhurio, vituo vya afya |
| **Watoto/ wanafunzi yatima** | Mtoto/mwanafunzi ambaye amefiwa na mzazi mmoja au wote wawili. | Nyumbani/ kwenye kaya, mitaani, vituo vya kulelea watoto, shuleni | Wajumbe wa kamati inayohusika na Watoto Wanaoishi katika Mazingira hatarishi; wazazi/ walezi; kundirika; walimu; watoa huduma za jamii; Viongozi wa dini; viongozi wa jamii na mitaa; | Kutembelea makazi ya mtoto; kufanya uchunguzi; mahojiano; ripoti/taarifa rasmi; watoa taarifa za jamii, kutembelea vituo vya watoto yatima, shuleni |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Watoto/ wanafunzi wenye changamoto maalumu katika ujifunzaji** | Mtoto/mwanafunzi ambaye anakumbana na vikwazo vya kujifunza vinavyojidhihirisha katika uwezo duni wa kusikiliza, kufikiri, kuzungumza, kusoma, kuandika au kufanya Hisabati. | Nyumbani/ Kwenye kaya, Mtaani, vituo maalum vya kulelea watoto, shuleni, Vyuo vya kati na Vyuo Vikuu | Walimu, wahadhiri, wakufunzi, watoa huduma katika vituo vya upimaji wazazi/walezi | Uchunguzi na/au upimaji wa usomaji kwa sauti, kujieleza kwa maandishi, hesabu, kumbukumbu, lugha, tabia, stadi za jamii, stadi za mwili na ukuaji. |
| **Mtoto/ mwanafunzi mwenye Kipawa na Kipaji** | Mtoto/mwanafunzi mwenye Uwezo wa asili katika nyanja fulani ambapo anafanya kwa ufanisi zaidi ya wenzake. Inahusisha taaluma, sanaa, muziki na michezo.<br>Kiwango cha juu sana cha uwezo wa kiakili unaodhihirishwa katika kuwa na ufahamu wa haraka, ufahamu wa juu wa mambo ya msingi, uwezo wa kipekee katika kukabiliana na mambo magumu, kupenda mambo mbalimbali, kuwa na matarajio makubwa, tabia ya kutenda kwa usahihi n.k. | Nyumbani/ kwenye kaya, Shuleni, Vyuo vya mafunzo ya Ufundi stadi na Vyuo mbalimbali na Vyuo Vikuu, mitaani | Wazazi/Walezi; majirani; kundirika; walimu; wahadhiri, wakufunzi | Tathmini mbalimbali kama: Uchunguzi na upimajii juu ya (i) Majaribio ya Kikundi k.m., jaribio la kupima uwezo wa utambuzi, jaribio la kupima uwezo wa kufikiri (ii) uchunguzi wa kina wa tabia katika nyanja maalum. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Watoto/ wanafunzi wanaoishi katika umasikini uliokithiri** | Mtoto/mwanafunzi ambaye anaishi katika familia ambayo inashindwa kukudhi mahitaji ya lazima kama kupata chakula, malazi na mavazi. | Nyumbani/ kwenye kaya, shuleni, kwenye vituo vya afya, | Wajumbe wa kamati inayohusika na Watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi; viongozi wa jamii na mtendaji wa mtaa/ kijiji, majirani; kundirika; walimu; watoa huduma za jamii; viongozi wa dini; | Kutembelea makazi ya mtoto; kufanya uchunguzi; mahojiano; ripoti/taarifa rasmi; watoa taarifa za jamii, vijiji na rejista za kata, kutembelea shule |
| **Watoto wa kike na wa Kiume** | Mtoto wa kike au wa kiume anayepata vikwazo vya kuandikishwa na kushiriki katika ujifunzaji kutokana na jinsia yake.<br>. | Nyumbani/ kwenye kaya, mtaani, shuleni, vyuo vya kati na Vyuo Vikuu. | Wajumbe wa kamati inayohusika na Watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi; viongozi wa jamii na mitaa; majirani; kundirika; walimu; watoa huduma za jamii; viongozi wa dini; wahadhiri, wakufunzi nk | Kutembelea makazi ya mtoto; kufanya uchunguzi; mahojiano; ripoti/taarifa rasmi; watoa taarifa za jamii, vijiji na rejista za kata. kutembelea shuleni au vyuoni |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Watoto/ wanafunzi wanaoishi mbali na shule** | Watoto/wanafunzi wanaolazimika kutembea umbali mrefu zaidi ya kilomita 1.5 kwa (elimu za awali), kilomita 3 kwa (shule za msingi) na kilomita 5 kwa (shule za sekondari) ili kufika shuleni.<br><br>Watoto/wanafunzi wanaotembea na kupita katika mazingira hatarishi na ambao wanakabiliwa na hatari nyingine wakiwa njiani. | Nyumbani/ kwenye kaya, shuleni | viongozi wa jamii na mitaa; majirani; kundirika; walimu; watoa huduma za jamii; viongozi wa dini | Kutembelea makazi ya mtoto; kufanya uchunguzi; mahojiano; ripoti/taarifa rasmi; watoa taarifa za jamii, vijiji na rejista za kata, kutembelea shuleni |
| **Wanafunzi wenye ulemavu** | Watoto/wanafunzi wenye ulemavu wa; uziwi, baki ya usikivu, uziwikutoona, uoni, uoni hafifu, usonji, viungo, mawasiliano, akili, ualbino na ulemavu zaidi ya mmoja. | Nyumbani; katika kaya; mitaani; katika nyumba za kulelea watoto; kwenye kituo cha afya. shuleni | Wazazi/Walezi, wajumbe wa kamati inayohusika na watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi, timu ya watoa huduma za upimaji, kundirika Maafisa Ustawi wa Jamii, Maafisa Maendeleo ya Jamii, walimu, wahadhiri, wakufunzi, Viongozi wa jamii na Mitaa, viongozi wa vyama/Mashirika ya Watu Wenye Ulemavu (DPO), ripoti/taarifa rasmi, watoa taarifu za jamii. Watendaji wa kata/ mitaa. | viashiria kwa ajili ya uchunguzi, ripoti/ taarifa rasmi, kutembelea nyumbani/ makazi ya mtoto. Kutembelea shuleni na vyuoni |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Watoto wanaokinzana na sheria** | Mtoto (chini ya umri wa miaka 18) ambaye anakabiliwa na mfumo wa vyombo vya usimamizi wa sheria kwa sababu ya kushukiwa au kutuhumiwa kutenda kosa/uhalifu kama vile ubakaji, mauaji, ukatili wa kijinsia; wizi, uporaji, utapeli; n. k | Gerezani; kituo cha polisi; kizuizini (mahabusu ya watoto); ofisi ya ustawi wa jamii; ofisi ya serikali ya kijiji/ mtaa | Wajumbe wa Kamati inayohusika na watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi, Dawati la jinsia na watoto la polisi; Maafisa Ustawi wa Jamii; wazazi/walezi; majirani; kundirika; walimu. Watoa huduma wengine wa jamii; Afisa Maendeleo ya Jamii; viongozi wa dini; viongozi wa jamii na mitaa/vijiji | Kutembelea magerezani na vizuizini (mahabusu ya watoto); kufanya uchunguzi/ ukaguzi/mapitio ya rejista/ripoti za polisi; majalada ya watoto; rekodi za mfumo wa usimamizi wa kesi za halmashauri, kutembelea shule |
| | Mtoto aliyezaliwa gerezani au aliambatana na mama yake gerezani. | | | |
| | Mtoto anayedaiwa kufanya uhalifu, yuko chini ya ulinzi wa polisi, gerezani, au kizuizini. | | | |

## 2.2 Ubainishaji, upimaji, utoaji wa afua stahiki na tathmini

Utaratibu wa ubainishaji, upimaji, na utoaji wa afua stahiki kwa watoto wenye mahitaji maalumu umegawanyika katika hatua kuu nne kama ifuatavyo:

### 2.2.1 Hatua ya Kwanza: Ubainishaji

Utaratibu wa ubainishaji wa watoto/wanafunzi wenye mahitaji maalumu ya kielimu unapaswa kutekelezwa na wataalamu kwa kushirikiana na jamii. Aidha, ubainishaji wa watoto/wanafunzi wenye mahitaji maalumu utakuwa endelevu kwa kusimamiwa na mamlaka ya ngazi husika.

Ubainishaji wa watoto/wanafunzi wenye mahitaji maalumu ya kielimu utafanyika kwa kuzingatia utaratibu ufuatao:

i. Timu ya ubainishaji kukutana na kuandaa mpango kazi

ii. Kupitia malengo na utaratibu wa ubainishaji

iii. Kuandaa zana na vituo vya kufanyia ubainishaji

iv. Kuendesha kampeni za uhamasishaji kwa jamii kuhusu ubainishaji

v. Kutekeleza zoezi la ubainishaji

vi. Kuchambua taarifa za ubainishaji na kuandika ripoti

vii. Kuwasilisha ripoti ya ubainishaji katika mamlaka zinazohusika

#### 2.2.1.1 Taarifa zinazopaswa kukusanywa na kusajiliwa.

Timu ya ubainishaji inapaswa kujaza Fomu A1 ya taarifa ya mtoto/mwanafunzi iliyopewa jina la Fomu ya Ubainishaji wa Awali (Angalia Kiambatisho cha 1). Viashiria vya awali vya uwepo wa mahitaji maalumu vinapobainika, timu ya ubainishaji inapaswa kujaza taarifa ya mtoto/mwanafunzi na kumpa rufaa ya kwenda kwenye vituo vya upimaji.

Katika ngazi ya shule za msingi, mpango wa ubainishaji unapaswa kufanywa kwa kumshirikisha mzazi/mlezi ambapo Fomu B1 yenye taarifa za mtoto/mwanafunzi inajazwa na kukamilika (Angalia Kiambatisho cha 1). Mchakato huu unapaswa kuzingatiwa katika vyuo vya kati na vyuo vikuu mara tu ubainishaji utakapofanyika. Wazazi/walezi wahusishwe pale inapowezekana.

Hatua hii ya ukusanyaji taarifa inapaswa kutekelezwa kwa umakini ili kupata hitimisho sahihi la ubainishaji na rufaa.

### 2.2.2 Hatua ya Pili: Upimaji

Baada ya taarifa ya mtoto/mwanafunzi kujazwa na kukamilika (Hatua ya Kwanza) na kuthibitishwa kwamba mtoto/mwanafunzi anahitaji huduma ya ziada, upimaji utafanyika ili kuweza kupata uelewa wa kina wa mahitaji ya kielimu ya mtoto/mwanafunzi (Angalia Fomu C1). Hii inafanyika kwa kutumia ushuhudiaji, kumbukumbu ya maelezo kutoka kwenye jalada la mtoto/mwanafunzi, madaftari ya mazoezi na taarifa za mdomo/maandishi kutoka kwa wazazi/walezi, walimu au wahadhiri. Upimaji unapaswa kufanyika katika Vituo vya upimaji ili kubaini mahitaji ya Kielimu.

Upimaji wa watoto/wanafunzi wenye mahitaji maalumu ya kielimu utafanyika kwa kuzingatia utaratibu ufuatao:

i. Kumpokea mtoto/mwanafunzi kutoka vituo vya ubainishaji (nyumbani, shuleni/chuoni au hospitalini).

ii. Kujaza taarifa za awali za mtoto/mwanafunzi katika fomu ya usajili

iii. Kuchukua historia ya mtoto/mwanafunzi kwa lengo la kubaini eneo lenye changamoto.

iv. Kufanya upimaji wa kina katika eneo/maeneo husika

v. Kujaza taarifa ya upimaji kwa kila eneo

vi. Kuwasilisha, kujadili na kuunganisha taarifa za upimaji kwenye jopo

vii. Kutoa mapendekezo kutokana na matokeo ya upimaji

viii. Kuwasilisha taarifa kwa mamlaka husika

### 2.2.3 Hatua ya Tatu: Utoaji wa Afua stahiki

Taarifa iliyotolewa katika Hatua ya Pili itasiadia katika utoaji wa afua stahiki kwa watoto/wanafunzi wenye mahitaji maalumu ya kielimu. Utoaji wa afua stahiki utazingatia utaratibu ufuatao:

i. Kupokea taarifa ya mahitaji ya kielimu na vifaa saidizi kutoka vituo vya upimaji

ii. Kuandaa Mpango Binafsi wa Ujifunzaji/afua stahiki kwa kushirikiana na mzazi/mlezi

iii. Kutekeleza mpango wa afua stahiki/Mpango Binafsi ya Ujifunzaji kwa kushirikiana na mzazi/mlezi

iv. Kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mpango Binafsi wa Ujifunzaji/Afua Stahiki kwa kushirikiana na mzazi/ mlezi

v. Kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa utoaji wa afua stahiki kwenye mamlaka husika.

### 2.2.4 Hatua ya Nne: Ufuatiliaji na Tathmini

i. Ufuatiliaji na tathmini ya utoaji wa afua stahiki kwa mtoto/mwanafunzi kwa kuzingatia mahitaji yake maalumu ya kielimu utafanywa angalau mara nne kwa mwaka kwa kutumia wakuu wa shule, maafisa elimu kata, wilaya, mikoa na ngazi ya taifa pamoja na wathibiti ubora wa shule na vyuo.

ii. Kupokea taarifa za utekelezaji wa afua stahiki

iii. Kupitia upya na kuchambua taarifa za utekelezaji wa afua stahiki

iv. Kupendekeza uboreshaji wa utekelezaji wa afua stahiki

v. Kuwasilisha taarifa ya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa afua stahiki

# SURA YA TATU

## 3.0 Uundaji wa Timu za Ubainishaji

Sura hii inaelekeza namna ya kuunda timu za ubainishaji na upimaji katika ngazi za taifa, mkoa, halmashauri, kata, kijiji/mtaa na taasisi za kielimu ngazi zote. Aidha, sura hii inaelelekeza wataalamu wanaohusika katika uundaji wa timu.

Timu za ubainishaji na upimaji zitajumuisha watu wenye ujuzi na/au taaluma mbalimbali wanaopatikana katika ngazi ya taifa, mkoa, halmashauri, kata, kijiji/mtaa na taasisi za kielimu ngazi zote. Katika ngazi ya shule, vyuo vya elimu ya kati na vyuo vikuu, kuwepo na timu ya walimu na watumishi mwega watakaopatiwa mafunzo ya ubainishaji wa awali. Aidha, katika ngazi ya kata kuwepo na timu ya ubainishaji wa awali itakayoratibu ubainishaji katika ngazi za vijiji/mitaa.

## 3.1 Muundo wa Timu ya Ubainishaji na Upimaji

### 3.1.1 Ngazi ya Taifa

Timu ya ubainishaji na upimaji ngazi ya taifa itajumuisha walimu wataalamu katika maeneo ya kitaaluma ya ulemavu wa akili/usonji, uoni, uziwi, uziwikutoona, matamshi, viungo, afya, ustawi wa jamii, saikolojia na unasihi.

### 3.1.2 Ngazi ya Mkoa

Timu ya ubainishaji na upimaji ngazi ya mkoa itajumuisha; Afisa elimu ya watu wazima na elimu nje ya mfumo rasmi;

walimu wataalamu katika maeneo ya kitaaluma ya ulemavu wa akili/usonji, uoni, uziwi, uziwikutoona, matamshi, viungo, afya, ustawi wa jamii, saikolojia na unasihi.

### 3.1.3 Ngazi ya Halmashauri

Timu ya ubainishaji na upimaji ngazi ya mkoa itajumuisha; Afisa elimu - elimu maalumu (Msingi na Sekondari), walimu wataalamu katika maeneo ya kitaaluma ya ulemavu wa akili/usonji, uoni, uziwi, uziwikutoona, matamshi, viungo, afya, ustawi wa jamii, saikolojia na unasihi.

### 3.1.4 Ngazi ya Kata

Timu ya ubainishaji ngazi ya kata itajumuisha Afisa Elimu Kata, Afisa Ustawi wa Jamii, Afisa Maendeleo ya Jamii, Mganga/Muuguzi kutoka katika kituo cha afya/zahanati, mwakilishi wa kamati za huduma za jamii na walimu wataalamu katika maeneo ya kitaaluma ya ulemavu wa akili/usonji, uoni, uziwi, uziwikutoona au matamshi. Aidha, katika ngazi ya kata; timu ya ubainishaji itaratibu ubainishaji katika ngazi za vijiji/mitaa.

### 3.1.5 Ngazi ya taasisi za kielimu

Timu ya ubainishaji na upimaji ngazi ya taasisi za kielimu (vyuo vikuu, vyuo vya elimu ya kati (chini ya NACTVET), vyuo vya ualimu, shule za sekondari na msingi) itajumuisha; walimu wataalamu katika maeneo ya kitaaluma ya ulemavu wa akili/usonji, uoni, uziwi, uziwikutoona, matamshi, viungo, afya, ustawi wa jamii, saikolojia na unasihi.

# SURA YA NNE

## 4.0 Majukumu na Wajibu wa Watumiaji wa Mwongozo

Sura hii inafafanua majukumu na wajibu wa watumiaji wa mwongozo huu wakiwemo watendaji wa Wizara, Mikoa, Halmashauri, Kata, Vijiji/Mitaa, Shule na Vyuo, wadau na wabia wanaohusika katika ubainishaji na upimaji wa watoto/wanafunzi wenye mahitaji maalumu ya kielimu.

## 4.1 Ngazi ya Wizara

### 4.1.1 Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (WyEST)

WyEST itatekeleza majukumu yafuatayo:

i. Kuwajengea uwezo watekelezaji wa mwongozo;

ii. Kusambaza mwongozo kwa wadau kwa ajili ya utekelezaji;

iii. Kusimamia ubora wa shughuli za ubainishaji na upimaji wa watoto/wanafunzi wenye mahitaji maalumu nchini;

iv. Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mwongozo; na

v. Kuhamasisha wadau kuchangia utekelezaji wa mwongozo.

### 4.1.2 Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI)

OR-TAMISEMI itatekeleza majukumu yafuatayo:

i. Kusimamia utekelezaji wa mwongozo katika mamlaka zilizopo chini yake;

ii. Kuratibu shughuli zinazotekelezwa na wadau wa elimu wanaotekeleza programu/miradi ya ubainishaji na upimaji wa watoto/wanafunzi wenye mahitaji maalumu;

iii. Uimarishaji/uanzishaji, uendeshaji na usimamizi wa vituo vya ubainishaji na upimaji wa watoto/wanafunzi wenye mahitaji maalumu; na

iv. Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya uendeshaji wa vituo vya upimaji na kampeni za ubainishaji wa watoto wenye mahitaji maalumu katika ngazi ya shule na jamii.

### 4.1.3 Ngazi ya Mkoa

Mamlaka ya mkoa katika mwongozo huu itatekeleza majukumu yafuatayo:

i. Kusimamia utekelezaji wa mwongozo katika mamlaka zilizopo chini yake;

ii. Kuratibu shughuli zinazotekelezwa na wadau wa elimu wanaotekeleza programu/miradi ya ubainishaji na upimaji wa watoto/wanafunzi wenye mahitaji maalumu;

iii. Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya uendeshaji wa vituo vya upimaji na kampeni za ubainishaji wa watoto

wenye mahitaji maalumu katika ngazi ya shule na jamii; na

iv. Kuimarisha/kuanzisha, kuendesha na kusimamia kituo cha upimaji cha Mkoa.

### 4.1.4 Ngazi ya Halmashauri

Mamlaka katika ngazi ya halmashauri itatekeleza majukumu yafuatayo:

i. Kuteua wataalamu watakaounda timu za ubainishaji na upimaji wa watoto/wanafunzi wenye mahitaji maalumu ya kielimu;

ii. Kusimamia utekelezaji wa mwongozo katika shule za msingi na sekondari, na kata vijiji/mitaa;

iii. Kuratibu mafunzo elekezi ya ubainishaji kwa timu za utekelezaji katika ngazi za chini ya mamlaka yake;

iv. Kuratibu shughuli za wadau wa elimu maalumu na jumuishi wanaotekeleza shughuli za ubainishaji na upimaji wa watoto/wanafunzi wenye mahitaji maalumu;

v. Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya uendeshaji wa vituo vya upimaji na kampeni za ubainishaji wa watoto wenye mahitaji maalumu katika ngazi ya shule na jamii,

vi. Kuanzisha na kuendesha kituo cha upimaji katika ngazi ya halmashauri, na

vii. Kutayarisha na kutunza kanzi data ya watoto/wanafunzi wenye mahitaji maalumu waliobainishwa na kupatiwa afua stahiki.

### 4.1.5 Ngazi ya Kata

Mamlaka ya Serikali ngazi ya Kata katika mwongozo huu itatekeleza majukumu yafuatayo:

i. Kutoa ushauri kwa timu za vijiji/mitaa zinazohusika na ubainishaji;

ii. Kwa kushirikiana na timu za vijiji/mitaa, kufanya ziara/kutembelea kaya na familia kwa ajili ya kubaini watoto wenye umri wa kwenda shule wenye mahitaji maalumu ili waweze kuandikishwa;

iii. Kuungana na afisa ustawi wa jamii katika ngazi ya kata kwa ajili ya kubaini watoto/wanafunzi na familia zinazoishi katika umaskini uliokithiri, watoto/wanafunzi yatima na makundi yaliyo katika mazingira hatarishi;

iv. Kuratibu mafunzo elekezi kwa walimu katika ngazi ya shule za msingi na sekondari;

v. Kupokea rufaa kutoka ngazi ya kijiji/mtaa na kuwapeleka watoto/wanafunzi kwa watoa huduma wengine kama inavyohitajika;

vi. Kuratibu shughuli za ubainishaji zinazofanywa na wadau watoa huduma katika ngazi ya kata;

vii. Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa shughuli za ubainishaji; na

